FUNZO LA 36

1. Je, Musa alipokuwa akizungumza na Mungu juu ya mlima, Waisraeli walifanya nini chini ya mlima?
-Waisraeli walimtengeneza ndama wa dhahabu na wakamwabuda.

2. Je, Mungu alijua kuwa Waisraeli waliabudu ndama wa dhahabu?
-Ndiyo.

3. Je, Mungu alikasirishwa na Waisraeli?
-Mungu alikasirishwa sana na Waisraeli.
-Mungu alikarishwa sana na Waisraeli hadi alitaka kuwaharibu.

4. Je, kwa nini Mungu hakuwaharibu Waisraeli wote?
-Kwa sababu Musa alimuomba Mungu asiwaharibu.

5. Je, Musa alifanya nini alipofika chini ya mlima?
-Musa alikasirishwa sana na Waisraeli hadi akatupa chini na kuvunja zile mbao mbili za mawe ambazo zilikuwa na amri za Mungu.

6. Kwa sababu Musa alivunja zile mbao mbili za mawe ambazo Mungu aliandika amri zake, je, Mungu alimwambia nini Musa?
-Mungu alimwambia Musa achonge mbao mbili zingine na apeleke mlimani ili Mungu aandike tena zile amri kumi.



7. Je, iwapo Waisraeli wasingejenga ile hema hakika kama alivyosema Mungu, utukufu wake ungeingia ndani yake?
-La.

8. Je, Waisraeli walipaswa kumwendea Mungu kwa njia yao?
-La.

9. Je, ni kwa njia ipi Waisraeli walipaswa kumwendea Mungu?
-Kwa njia ya Mungu.

10. Je, twawezaje kujua njia ya Mungu?
-Kupitia kwa kitabu cha Mungu, Biblia.

-Mungu alimchagua Musa kuwaongoza Waisraerli kutoka Misri na kutoka utumwani.

-Musa pia alikuwa mjumbe wa Mungu.

-Mungu alipotaka kuzungumza na Waisraeli, alizungumza na Musa kisha Musa akawaambia Waisraeli.

-Mungu alimuelekeza Musa kuwaambia Waisraeli kile alichosema Mungu.

-Pia Mungu alimuelekeza Musa kuandika kile alichota Mungu kiandikwe.

-Je, ni nani aliyeandika vitabu tano vya kwanza vya Biblia?

-Musa.

-Je, Musa alijuaje alichopaswa kuandika?

-Mungu alimuelekeza Musa kuandika kile ambacho Mungu alitaka kiandikwe.

-Waisraeli walikuwa wametoka Misri na walikuwa wakisafiri kupitia jangwani.

-Je, Waisraeli walipokuwa wakisafiri katika jangwa, walijuaje njia waliostahili kufuata?

-Mungu aliwaongoza.

Tusome Kutoka 40:36-38

36-Na hapo lile wingu lilipoinuliwa kutoka juu ya maskani, wana wa Israeli wakaenda mbele katika safari zao zote,
37-bali kama lile wingu halikuinuliwa, wakati ule hawakusafiri hata siku ile lilipoinuliwa tena.
38-Kwa maana lile wingu la Bwana lilikuwa juu ya maskani wakati wa mchana, na mlikuwa na moto ndani yake wakati wa usiku, mbele ya macho ya nyumba ya Israeli katika safari zao zote.

-Mungu alipokuwa akitaka Waisraeli wasimame, aliagiza wingu lisimame.

-Mungu alipotaka Waisraeli waondoke, alifanya lile wingu likaondoka.



-Baada ya Mungu kuwapa Waisraeli amri kumi na Waisraeli kumjengea Mungu hema, Mungu aliinua lile wingu.

-Je, Mungu alikuwa akiwaelekeza wapi Waisraeli?

-Mungu alikuwa akiwaongoza Waisraeli kuelekea Kanaani, nchi aliyoahidi baba yao Ibrahamu.

-Waisraeli walifuata lile wingu na Mungu akawaongoza hadi mpaka wa Kanaani.

-Waisraeli walipofika katika mpaka wa Kanaani, Mungu alimwambia Musa afanye nini?

Tusome Hesabu 13:1-2

1-Kisha Bwana akanena na Musa, akamwambia,
2-Tuma watu, ili waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani, niwapayo wana wa Israeli; katika kabila ya baba zao mtamtuma mtu mmoja, kila mtu na awe mkuu kati yao.

-Mungu alimwambia Musa achangue mtu mmoja kutoka kila kabila ya Israeli ili wakaipeleleze ile nchi.

-Musa alimtii Mungu na akawatuma wale wanaume kumi na wawili wakaipeleleze nchi ya Kanaani.

Tusome Hesabu 13:3

3-Basi Musa akawatuma kutoka nyika ya Parani kama alivyoagizwa na Bwana; wote walikuwa ni watu walio vichwa vya wana wa Israeli.

-Je, kabla ya Musa kuwatuma wale kumi na wawili wakaipeleleze ile nchi, aliwaambia nini?

Tusome Hesabu 13:17-21

17-Musa akawapeleka ili waipeleleze nchi ya Kanaani, akawaambia, Pandeni sasa katika Negebu mkapande milimani,
18-mkaitazame nchi ni ya namna gani; na watu wanaokaa ndani yake, kwamba ni hodari au dhaifu, kwamba ni wachache au wengi;
19-na nchi wanayoikaa kwamba ni njema au mbaya; kwamba wanakaa katika matuo au katika ngome;
20-nayo nchi ni ya namna gani, kwamba ni nchi ya unono au ya njaa, kwamba ina msitu au sivyo. Iweni na moyo mkuu, mkayalete matunda ya nchi. Basi wakati ule ulikuwa wakati wa kuiva zabibu za kwanza.
21-Basi wakapanda wakaipeleleza nchi toka jangwa la Sini hata Rehobu, mpaka kuingia Hamathi.

-Baada ya siku arubaini, wale kumi na wawili walirejea kutoka kupeleleza nchi ya Kanaani.

-Hiki ndicho wale kumi na wawili walichomwambia Musa na Waisraeli kuhusu ile nchi ya Kanaani.

Tusome Hesabu 13:27-29



27-Wakamwambia wakasema, Tulifika nchi ile uliyotutuma, na hakika yake, ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali, na haya ndiyo matunda yake.
28-Lakini watu wanaokaa katika nchi ile ni hodari, na miji yao ina maboma, nayo ni makubwa sana; na pamoja na hayo tuliwaona wana wa Anaki huko.
29-Amaleki anakaa katika nchi ya Negebu; na Mhiti, na Myebusi, na Mwamori wanakaa katika milima, na Mkanaani anakaa karibu na bahari; na kando ya ukingo wa Yordani.

-Nchi ya Kanaani ilikuwa nchi ya asali na maziwa.

-Ilikuwa pia ni nchi iliyojawa na watu wakubwa na wenye nguvu.

-Miji ya Kanaani pia ilikuwa dhabiti, ilikuwa imezungukwa na kuta zilizo juu.

-Kati ya wale kumi na wawili walioenda kupeleleza nchi, kumi kati yao hawakumwamini Mungu.

-Je, wale kumi ambao hawakumwamini Mungu waliwaambia nini Waisraeli?

Tusome Hesabu 13:31-33

31-Bali wale watu waliopanda pamoja naye wakasema, Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi.

32-Wakawaletea wana wa Israeli habari mbaya ya ile nchi waliyoipeleleza, wakasema, Ile nchi tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi inayowala watu wanaoikaa; na watu wote tuliowaona ndani yake ni watu warefu mno.

33-Kisha, huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anaki, waliotoka kwa hao Wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi.

-Je, kwa nini wale kumi ambao hawakumwamini Mungu hawakutaka kwenda Kanaani?

-Wale kumi waliogopa watu wakubwa na wenye nguvu waliokuwa wakiishi Kanaani.

-Wale kumi hawakuamini kuwa Mungu alikuwa na uwezo wa kuwashinda watu walioishi Kanaani.

-Wale kumi hawakuamini ahadi ya Mungu ya kuwapa Israeli nchi ya Kanaani.

-Wale kumi waliwaambia Waisraeli kuwa wasiingie Kanaani.
-Kati ya wale kumi na wawili, wawili walimwamini Mungu.

-Majina yao yalikuwa ni Kalebu na Yoshua.
-Je, Yoshua na Kalebu waliwaambia nini Waisraeli?

Tusome Hesabu 13:30

30-Kalebu akawatuliza watu mbele ya Musa, akasema, Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila



shaka.

-Je, kwa nini Yoshua na Kalebu walitaka kuingia nchi ya Kanaani?

-Kalebu na Yoshua hawakuogopa watu wakubwa na wenye nguvu waliokuwa katika nchi ya Kanaani.

-Kalebu na Yoshua waliamini kuwa Mungu ni mwenye nguvu zaidi na angewashinda watu waliokuwa wakiishi Kanaani.

-Kalebu na Yoshua waliamini ahadi ya Mungu ya kuwapa Waisraeli nchi ya Kanaani.

-Kalebu na Yoshua waliwaambia Waisraeli wamtii Mungu na waingie Kanaani.

-Je, Israeli waliamini wale kumi wasiomwamini Mungu au waliwaamini Yoshua na Kalebu ambao walimwamini Mungu?

Tusome Hesabu 14:1-4

1-Mkutano wote wakapaza sauti zao wakalia; watu wakatoka machozi usiku ule.

2-Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili.

3-Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka; je!

Si afadhali turudi Misri?
4-Wakaambiana, Na tumweke mtu mmoja awe akida, tukarudi Misri.

-Waisraeli waliwaamini wale kumi wasiomwamini Mungu na ambao hawakutaka kuingia Kanaani.

-Kalebu na Yoshua wakanena tena na Waisraeli.

Tusome Hesabu 14:6-9

6-Na Yoshua mwana wa Nuni, na Kalebu mwana wa Yefune, waliokuwa miongoni mwao walioipeleleza nchi, wakararua nguo zao;
7-wakanena na mkutano wote wa wana wa Israeli wakasema, Nchi ile tuliyopita kati yake ili kuipeleleza, ni nchi njema mno ya ajabu.
8-Ikiwa Bwana anatufurahia, atatuingiza katika nchi hii atupe iwe yetu, nayo ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali.
9-Lakini msimwasi Bwana, wala msiwaogope wale wenyeji wa nchi, maana wao ni chakula kwetu; uvuli uliokuwa juu yao umeondolewa, naye Bwana yu pamoja nasi; msiwaogope.

-Kalebu na Yoshua waliwasii Waisraeli wasikose kumtii Mungu.

-Kalebu na Yoshua waliwaambia Waisraeli kuwa Mungu alikuwa mwenye nguvu zote za kuwashinda watu wa Kanaani.



-Je, Waisraeli walikubali kuingia Kanaani?

Tusome Hesabu 14:10a

10-Lakini mkutano wote wakaamuru wapigwe kwa mawe.

-Waisraeli bado hawakutaka kuingia Kanaani.
-Waisraeli bado hawakutaka kumtii Mungu.
-Waisraeli walitaka kuwapiga mawe Kalebu, Yoshua na Musa.

-Je, Mungu alisikia walichokuwa wakisema Waisraeli?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alijua kuwa Waisraeli hawakutaka kuingia Kanaani?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alijua kuwa Waisraeli hawakuamini kuwa alikuwa na nguvu za kuweza kuwashinda watu wa Kanaani?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alijua kuwa Waisraeli hawakuamini ahadi yake ya kuwapa Kanaani?
-Ndiyo.

-Waisraeli hawakuamini kuwa Mungu angetimiza ahadi yake ya kuwapa Kanaani.

-Je, iwapo hatutaamini ujumbe wa Mungu, tunamwitaje Mungu?

-Muongo.
-Waisraeli hawakuamini ujumbe wa Mungu.
-Waisraeli walimwita Mungu muongo.

-Yafuatacho ndicho Mungu aliyosema:

Tusome Hesabu 14:26-32

26-Kisha Bwana akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia,
27-Je!  Nichukuane na mkutano mwovu huu uninung'unikiao hata lini?  Nimesikia manung'uniko ya wana wa Israeli, waninung'unikiayo.
28-Waambieni, Kama niishivyo, asema Bwana, hakika yangu kama ninyi mlivyonena masikioni mwangu, ndivyo nitakavyowafanyia ninyi;
29-mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili, na wote waliohesabiwa miongoni mwenu, kama jumla ya hesabu yenu, tangu waliopata umri wa miaka ishirini na zaidi, hao walioninung'unikia,
30-hakika yangu hamtaingia ninyi katika nchi, ambayo niliinua mkono wangu ya kwamba nitawaketisha humo, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, na Yoshua mwana wa Nuni.
31-Lakini Watoto wenu, ambao mlisema watakuwa mateka, ndiyo nitakaowaleta na kuwatia ndani, nao wataijua nchi ninyi mliyoikataa.



32-Lakini katika habari zenu, mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili.

-Je, kwa sababu Waisraeli walikataa kumwamini Mungu, ni nani pekee aliyekubaliwa kuingia Kanaani?

-Ni Kalebu, Yoshua na watoto wa Waisraeli.

-Je, kwa sababu Waisraeli walikataa kumtii Mungu, Mungu aliwaadhibu vipi Waisraeli?

-Hawakuingia Kanaani.
-Wote walikufa jangwani.

-Mungu huwaadhibu kwa kifo wote wasiomwamini.

-Watu wa wakati wa Nuhu walikataa kumwamini Mungu, Mungu aliwaadhibu kwa kifo.

-Watu wa Sodoma na Gomora walikataa kumwamini Mungu, Mungu aliwaadhibu kwa kifo.

-Farao na Wamisri walikataa kumwamini Mungu, Mungu aliwaadhibu kwa kifo.

-Mungu atawaadhibu kwa kifo katika Ziwa la Moto wa Milele wote wasiomwamini.